

# **TAASISI YA BIBLIA NA UTUMISHI**

*Sangasanga Morogoro. Novemba 02, 07, 2015*

**Mada: WITO NA SIFA ZA KIONGOZI - MTUMISHI**

**I: Kiongozi – Mtumishi lazima awe na uhakika na wito wake.**

- Lazima atumike na kuongoza akiwa na uhakika na wito wake. Cf. Kutoka 21:1-6, Kumb. 15:12, 16, Rum. 1:1.

**II: Kiongozi – Mtumishi anapaswa kuwa na sifa zipi:-**

- Awe amejitoa kwa Bwana wake kikamilifu.
- Ana mtii Bwana wake kikamilifu.
- Anamtegemea Bwana wake kwa mambo yote.
- Wajibu wake mkuu ni kutenda mapenzi ya Bwana wake.
- Hataona aibu kuitwa mtumishi wa Bwana wake.
- Kama kiongozi anapaswa kujua lengo na mwelekeo wa watu wake.
- Kama kiongozi lazima atambue wajibu alionao kuwaongoza wengine na kuendeleza vipawa vyao.
- Kama kiongozi awe tayari wakati mwingine kuwa mpweke na kulaumiwa kwa makosa ya wengine.
- Kama kiongozi asione aibu kuomba msamaha inapobidi kufanya hivyo.
- Kama kiongozi asiingize siasa kuongoza watu wake. Cf. 1Kor. 4:16.
- Kama kiongozi awe na ujasiri kuchukua maamuzi magumu yatayohitaji ujasiri katika ulimwengu wa imani.
- Kama kiongozi aongoze kwa misingi ya Neno la Mungu.

**III: Majumuisho ya mada hii.**

- Kiongozi wa kiroho anapaswa kuwa mtumishi, kuwatumikia wale anaowaongoza.
- Ataongoza kwa misingi ya Neno la Mungu.
- Ataongoza kwa kujitunza nafsi yake mwenyewe na hivyo kuwa mfano wa kuigwa.
- Atalea na kutunza vipawa/karama za wale anaowaongoza.
- Ataongoza kwa kuhubiri, kufundisha na kushauri.